

MKATABA WA UPANGAJI

KATI YA

ENOCK GORDON MWAIPAJA
(Mwenye Majengo)

NA

SONGWE RIVERBANK ENTERPRISE
(Mpangaji)

MKATABA WA UPANGISHAJI WA MAJENGO

Umefanyika leo tarehe08..... mwezi.....02..... 2022

KATI YA

ENOCK GORDON MWAIPAJA wa MBEYA, ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu

NA

SONGWE RIVERBANK ENTERPRISE wa Mbeya ambaye kwa madhumini ya mkataba huu utajulikana kama MPANGAJI, kwa upande mwingine.

KWA KUWA MWENYE NYUMBA ni mmiliki/msimamizi/ mwangalizi halali wa Nyumba iliyopo katika JIJI LA MBEYA - maeneo ya FOREST MPYA na anayo nia ya kupangisha majengo hayo na;

KWA KUWA MPANGAJI anayo nia na yuko tayari kupanga nyumba hiyo

BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:

- i. Kwamba kodi ya Majengo hayo itakuwa ni shilingi za kitanzania Laki tano (500,000/=) tu kwa mwezi
- ii. Kwamba mpangaji atalazimika kulipa kodi hiyo kwa kipindi cha miezi sita kwa mkupuo mmoja yaani milioni tatu (3,000,000/=)
- iii. Kwamba mkataba huu utatumika katika kipindi cha miaka Mitano yaani toka 01/02/2022 mpaka 31/12/2027
- iv. Kwamba Mpangaji au Mwenye Majengo akiwa na nia ya kutokuendelea kipindi cha pili cha Mkataba atatoa Notisi ya Mwaka Mmoja (miezi 12) ili kuupa upande wa pili nafasi ya kutafuta mtu mwingine au sehemu nyingine na kuepuka hasara na usumbufu
- v. Kwamba malipo ya umeme na maji yako nje ya kodi tajwa hapo juu na italipwa kwa kutegemea hali halisi ya kiwango na matumizi ya mpangaji
- vi. Kwamba mpangaji atafanya marekebisho ama aina yoyote ya matengenezo pale tu atakapokubaliana na mwenye Nyumba
- vii. Kwamba mpangaji atatumia Majengo hayo kwa Shughuli ya shule
- viii. Kwamba mpangaji hatatakiwa kuweka na ama kuingiza mtu kama mpangaji mwingine (sub lease) bila makubaliano na mwenye Nyumba
- ix. Kwamba mpangaji ahakikishe anakabidhi Majengo yakiwa katika hali nzuri na yakiwa yamelipiwa gharama zote zikiwemo za umeme na maji
- x. Kwamba mkataba huu utaongozwa na Sheria ya Mikataba (*The Law of Contract Act, 1961 R.E 2002*) ya Tanzania pamoja na sheria nyinginezo zinazo ongoza mahusiano ya kimkataba nchini Tanzania



xi. Kwamba endapo itatokea kutokuelewana, pande zote mbili zimekubaliana kutatua matazizo yao kwa njia ya mazungumzo ya amani kabla ya kutumia njia za kimahakama

Kwamba pande zote mbili zimekubaliana na masharti tajwa hapo juu na wanathibitisha nia na madhumuni yao ya kufuata maelekezo na / au masharti tajwa hapo juu kwa kuweka sahihi katika mkataba huu kama ilivyo hapa chini;

MWENYE NYUMBA

MPANGAJI

JINA: **ENOCK G. MWAIPAJA**

JINA: **SONGWE RIVERBANK ENTERPRISE**

SAHIHI 

SAHIHI 

SIMU 0754270897

SIMU 0755910494



MBELE YANGU

Jina MARY Gatuna

Sahihi 

Anuani J.L.P. Logg, N

Tarehe 08/02/2022

